JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

Juni, 2023

Dodoma



Edit with WPS Office

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za Simu

Mkuu wa Shule: 0756075296/ 0626375296.

Makamu Mkuu wa Shule: 0769490660/0742628430

Matron/Patron 0744754475

Shule ya Sekondari KAIGARA

S.L.P 253 MULEBA - KAGERA

Tarehe 12.06.2023

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….
……………………………………………..
S.L.P ……………………………………..
…………………………………………….

Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAIGARA HALMASHAURI YA MULEBA MKOA KAGERA MWAKA 2023/2024

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023. na atasoma tahasusi ya ……..……

Shule ya Sekondari KAIGARA ipo umbali wa Kilometa 1KM KASIKAZINI mwa Mji wa MULEBA Usafiri wa basi kutoka mjini hadi Shule ya sekondari KAIGARA unapatikana katika kituo cha mabasi MULEBA Nauli ni Shilingi 1000/= kwa pikipiki na Shilingi 1000/=kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 13/08/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13.08.2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31.08.2023



Edit with WPS Office

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Suruali mbili (2) nyeusi zenye urefu wa kufunika kisigino lakini siyo kuikanyaga**(iwe inchi 19 mzunguko wa chini)** iwe ya **HESHIMA (isiwe ya kubana).**

ii. Shati mbili nyeupe (aina ya tomato) mikono mirefu, zenye vishikizo vya kawaida na mfuko mmoja upande wa kushoto.

iii. Mkanda mweusi wa ngozi upana usiozidi inchi mbili (**usiwe namadoido**)

iv. Vazi baada ya saa za masomo (shamba dress) ni suruali nyeusi (2) na T-shirt (2) rangi ya kijani yenye nembo ya shule inapatikana shuleni .

v. Jozi 2 za viatu vyeusi vya ngozi visiwe buti. Viatu visiwe na madoido viwe na visigino vifupi na vyenye kufungwa kwa kamba.

vi. Soksi nyeusi jozi mbili au zaidi.

vii. Tai moja(1) nyeusi yenye mistari ya rangi nyeupe inapatikana shuleni .

viii. Sweta mmoja (1) rangi ya dark blue yenye nembo ya shule inapatikana shuleni.

ix. T- shirt **2** rangi ya **royal blue** yenye michirizi mweupe zenye kola zinapatikana shuleni

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 8 (*counter book Q3*)
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);

ORODHA YA VITABU KWA KILA TAHASUSI (COMBINATION)

PHYSICS REFERENCE BOOKS

1. Muncaster R, (1993) A – LEVEL PHYSICS 4th Ed, Nelson Thornes Ltd U.K
2. Metha V.k, (2013) S.Chand's principles of PHYSCICS for class XII 7th ED, S.Chand & Company Pvt.Ltd, New Delhi

CHEMISTRY REFERENCE BOOKS

1. Jain S.K, (2010), Conceptual chemistry for class xl s. Chand & company Ltd, New Delhi, India
2. Mkayula, L.L et al ( 1998), physical, chemistry. Volume 1, ( mzumbe Book Project) Mzumbe, Tanzania.
3. Bahl B.S et al (2009) Essential of physical chemistry S. Chad & company Ltd, New Delhi, India.



Edit with WPS Office

4. Ramsden. E.N(2000), A – level chemistry, 4th Ed, Nelson Thornes Ltd U.K

BIOLOGY REFERENCE BOOK.

1. Taylor D.J,(1999), Biology Science, 3rd Ed,Cambridge Unverstity PressLondon.

GEOGRAPHY BOOKS

1. Mcknight T, (2008) Physical Geography A L and scape appereciation prentice Hall USA.
2. Pritichard J, (1984), Physical Geography for Africa, Longman group U.K
3. Bunnet R,( 1973), General Geography in Diagram, Education Singapore.
4. Monkhouse, F(1975) Principal of physical Geography, Education Hodder, UK

GENERAL STUDIES

1. Understanding general studies 3rd Edition for advanced level ( JOANES BIGIRWAMUNGU)

iv. Dissecting kit kwa kila mwanafunzi.`
v. Scientific calculator.
vi. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo kulingana na vipimo vilivyopo katika shule husika.
vii. Mashuka Jozi 2,(light blue), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (light blue)
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

ANGALIZO: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.

2.3 Michango mbalimbali

Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

NB: MICHANGO YOTE ILIPWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE Na. 32001200071 jina la akaunti MDC KAIGARA SECONDARYSCHOOL- Tawi lolote la NMB, na mwanafunzi alete risiti iliyotumika kuweka fedha hizo bank na iwe na jina la Mwanafuzi.

3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule



Edit with WPS Office

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).



Edit with WPS Office

3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Aje na kadi ya Bima ya Afya kama anayo.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.



Edit with WPS Office

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa Shule ..............................................

Jina la Mkuu wa Shule STEPHANO R.ANATORY

Mhuri wa Mkuu wa Shule ......HEADMASTER KAIGARA SECONDARY SCHOOL P. O. Box 253, MULEBA Date:..............................

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule 0756075296/ 0626375296
- Makamu Mkuu wa Shule 0769490660/0742628430
- Mwandamizi Taaluma 0712297660
- Mwandamizi Malezi 0753393418



Edit with WPS Office

VIAMBATANISHO

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina Kamili la Mwanafunzi ……………………………………………………..……………………

2. Anwani ya nyumbani ……………………………………………………………..…………………

3. **Mahali ulipozaliwa,** (i) Wilaya……………………………………………………………………...

(ii) Tarafa……………………………………………………………………...

(iii) Kata ………………………………………………………………….…

(iv) Kijiji/Mtaa……………………………………………………………………

**4. (a) Shule ya Sekondari ulipotoka …………………………………………………………………..**

(b) Anwani ya Shule ulipotoka ………………………………………………………………………

(c ) Mwaka uliomaliza Shule ya Sekondari…………………………………………………………….

(d) Mchezo unaopendelea zaidi…………………………………………………………………….

**5. Dini …………………………………………………………………………………………………….**

6. **Wazazi** (i) Jina la baba……………………………………………………………………...

Anwani yake ……………………………………………………………….….

Namba ya simu ya mkononi ……………………………………………..….

Anaishi/ Amefariki (Kata isiyohusika)

Saini……………………………………………………………………………….

(ii) Jina la mama ……………………………………………………………..…...

Anwani yake ……………………………………………………………………

Namba ya simu ya mkononi …………………………………………………..

Anaishi/ amefariki (kata isiyohusika)

Saini……………………………………………………………………………

(iii) Jina la Mlezi (kama si baba au mama)

Anwani yake …………………………………………………………………….

Namba ya simu ya mkononi …………………………………………………..

Uhusiano wake na wewe ni ……………………………………………….....

(iv) Saini ya Mlezi ……………………………………………………………………

(v) Saini ya Mwanafunzi ……………………………………………………...



Edit with WPS Office

## MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi ……………………………………………….. nakiri kwamba sitoshiriki katika mgomo wowote, fujo yoyote, kuhudhuria kikao kisicho na idhini ya utawala katika mazingira yote ya shule na kwamba sitoshiriki makosa yoyote ya jinai.

Nikiwa mwenye akili timamu naapa sitojihusisha na utovu wowote wa nidhamu na nitafuata taratibu/sheria, ratiba kwa mjibu wa mipango ya shule. Na sitazungumza kauli yoyote ya kuchochea/kuhamasisha/kushinikiz /kushawishi uvurugaji wa amani ya Shule mtu/kikundi/mdahalo.Sitashiriki majadiliano/maandamano/mabishano yanayohatarisha amani ya shule.

Ikiwa nitatenda kinyume na niliyotaja hapo juu niwajibishwe kwa mujibu wa sheria za shule.

Jina la ukoo……………………… Jina la kati…………………….. Jina la kwanza …………………

Sahihi ………………………………….. Tarehe………………………..

UTHIBITISHO WA MZAZI/ MLEZI

Mimi……………………………………………Mzazi/mlezi wa…………………………………..…(mwanafunzi) nathibitisha kwamba mwanangu amesoma na kuelewa mkataba huu. Akienda kinyume na mkataba huu asimamishwe masomo mara moja na hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake.

Sahihi …………………………… tarehe ………………… namba za simu………………………..



Edit with WPS Office

# IJAZWE NA MZAZI/MLEZI NA KURUDISHWA SHULENI

ANWANI YA MLEZI

……………………………………
……………………………………
……………………………………
TAREHE…………………………

KUMB NA…………………………………..
MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI KAIGARA,
S.L.P 253,
MULEBA.

YAH: MALEZI YA MTOTO

MIMI ……………………………………………………………..KIDATO CHA………….……TAHASUSI YA ………………MWAKA……………

Nimesoma sheria na kanuani za shule Kumb.Na…………..na kuelewa.

Ninapenda kukuhakikishia kwamba mimi mzazi/mlezi wa mtoto tajwa niko tayari kusaidiana na shule katika jitihada zote za kumjengea mtoto wangu nidhamu ya dhati wakati wote awapo shuleni

Naahidi nitajitahidi kumwongoza kwenye masomo yake kulingana na taratibu za shule.

ZINGATIA:

i. Asikose kuhudhuria shuleni kama hakuna sababu ya msingi ya kumzuia na akikosa, apewe kibali toka kwa mzazi/mlezi wake bila hivyo hatapokelewa.

ii. Asijihusishe namatendo ya utoro, uzururaji, matumizi ya madawa ya kulevya na vitendo vinginevyo ambavyo vinaweza kumzuia kuendelea na shule.

iii. Asipuuze au kukataa kuhudhuria miradi ya shule, kama vile kilimo na kutunza usafi wa mazingira.

iv. Asijihusishe na migomo au ushawishi wowote unaoweza kuvunja amani ya shule kwani kwa kufanya hivyo atafukuzwa shule mara moja.

v. Akazanie masomo kwa lengo la kufaulu mitihani yake ya ndani nayanje.



Edit with WPS Office

………………………… ……………………
JINA KAMILI MZAZI/MLEZI SAHIHI

MULEBA DISTRICT COUNCIL
KAIGARA SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM DATE………………………………

NAME OF STUDENT…………………………………………………………………….

To medical office I/C of ……………………………………………District/Regional;/Referral/Designated Hospital: P.O.BOX ………………………………………………….

Please examine the above named in full as to his/he physical and mental fitness for being able to pursue years of Secondary school Education. In case of an acute Defect/disability in each category or subcategory may render the applicant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs:-

i. Blood pressure …………………………………………………………………………………
ii. Sickle cell test ………………………………………………………………………………….
iii. (a) Eyesight ………………………………………………………….…………………..

(b) Hearing ……………………………………………………........................................

(c ) Spleen ………………………………………………………………………………………

(d) Limps ……………………………………………………………………………………..

(e) Venereal diseases ……………………………………………………………………….

(f) Leprosy………………………………………………………………………………….

(g) Epilepsy……………………………………………………….…………………….

(h) Typhoid …………………………………………………………………………………

iv. Neuroses ………………………………………………….....................................
v. Other serious diseases…………………………………………………………………
vi. Pregnancy:…………………………………………………………………………………

General comment (s)…………………………………………………………………………………

Name……………………………………………………………………Signature……………………
Designation ……………………………………………………………………………………………
Official stamp………………………………………………………………………………………….
Date ……………………………………………………………………………………….

*ANGALIZO:Mzazi athibitishe kuwa vipimo hivi vimefanyika kikamilifu na siyo kujaza jina na sahihi ya mganga .Atakayegundulika shuleni kuwa hakuchukuwa vipimo kihalali atarudishwa nyumbani.*



Edit with WPS Office

Edit with WPS Office